



# JARIDA MAAALUM

Toleo la 18 | Machi, 2021

**OFISI YA WAZIRI MKUU**



**NDANI...**

## MAJALIWA: WATANZANIA TUWAPUUZE WASIOLITAKIA MEMA TAIFA

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amewataka Watanzania waendeleo kushikamana, kudumisha amani na wapuuzze kauli za chuki zinazotolewa.....

## WAZIRI MHAGAMA: JENGENI VIWANDA VYA VIRUTUBISHI VYA VYAKULA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Jenista Mhagama ameushauri.....



Ofisi ya Waziri Mkuu



owm\_tz



www.pmo.go.tz





## MAJALIWA: WATANZANIA TUWAPUUZE WASIOLITAKIA MEMA TAIFA

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amewataka Watanzania waendeleo kushikamana, kudumisha amani na wapuuze kauli za chuki zinazotolewa na watu wasioitakia mema nchi kuhusu afya ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwani ni mzima wa afya.

"Tuendeleo kufanya ibada na kupata mawaidha yanayohamasisha amani na utulivu. Rais Dkt. Magufuli ni mzima wa afya anaendeleo na majukumu yake wakati sisi wasaidizi wake tukizunguka kuwahudumia wananchi. Leo nimezungumza naye na anawasalimia."

Waziri Mkuu ametoa kauli hiyo (Ijumaa, Machi 12, 2021) baada ya kushiriki sala ya Ijumaa mjini Njombe, ambapo amesisitiza kuwa Rais anafanya

kazi kulingana na mpango kazi wake. Amesema wananchi wanatakiwa kushikamana na kuifanya nchi kuendeleo kuwa na amani na utulivu.

Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kuwasisitiza wananchi waendeleo kuliombea Taifa na wawapuuze baadhi ya Watanzania ambao hawapo nchini na wamekuwa wakitoa kauli za chuki kwa sababu hawapendi maendeleo ya nchi na wanatamani kuona Taifa likiporomoka.

"...Tuwapuuze baadhi ya Watanzania ambao wamejawa na chuki tu, wamejawa na husda tu na wanatamani kuwachonganisha na kutaka kushuhudia Taifa hili likiporomoka."

"Kuanzia juzi hata leo asubuhi nimeona Watanzania wenzetu wenye husda tena hawako ndani



wako huko wanashawishi vyombo vya Kimataifa viseme Rais wa Tanzania anaumwa kajifungia hizo ni chuki tu, husda tu.”

”Watanzania tulieni uongozi wenu upo imara na mafanikio tunayaona, kumzushia rais ugonjwa ni chuki, wanasema atoke aende wapi? Ulishamkuta siku moja anazurura Kariakoo? Rais anampango wake wa kazi si mtu wa kuzurura.”

Waziri Mkuu amesema Rais Dkt. Magufuli anawa-saidizi wake kuanzia ngazi ya Taifa hadi kijijini na kwamba anafanyakazi kulingana na mpangokazi wake, hivyo amewataka Watanzania waendeleo kuwa na amani huku wakiamini Serikali yao.

“

**Tuendeleo kufanya ibada na kupata mawaidha yanayohamasisha amani na utulivu. Rais Dkt. Magufuli ni mzima wa afya anaendelea na majukumu yake wakati sisi wasaidizi wake tukizunguka kuwahudumia wananchi. Leo nimezungumza naye na anawasalimia.”**



Baadhi ya Waumini wa Dini ya Kiislam wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakati alipozungumza baada ya kushiriki katika Ibada ya Ijumaa katika Msiki wa Ijumaa Njombe Mjini, Machi 12, 2021.



## MAJALIWA: SERIKALI ITAJENGA 'COLD ROOM' UWANJA WA NDEGE WA SONGWE

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema Serikali inatarajia kujenga chumba maalumu cha kuhifadhi baridi (cold room) katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Songwe kwa ajili ya kuhifadhia maparachichi pamoja na mazao mengine kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi.

Waziri Mkuu ametoa kauli hiyo (jumaa, Machi 12, 2021 wakati akizungumza na wananchi baada ya kutembelea shamba la mkulima wa parachichi Bw. Steven Mlimbira katika kijiji cha Maheve wilayani Njombe.

Pia, Waziri Mkuu ameziagiza Halmashauri zote za mkoa wa Njombe zinazolima zao la parachichi zianzishe vitalu vya kuotesha miche katika eneo la kuanzia ekari tatu na kuigawa bure kwa wakulima, lengo likiwa ni kuhamasisha wananchi wengi kulima zao hilo na kuongeza uzalishaji.

Kufuatia umuhimu za zao hilo, Waziri Mkuu amemuagiza Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mhandisi

Marwa Mwita Rubirya afuatilie maendeleo ya vikundi vya wakulima wa parachichi na kushirikiana nao katika kutatua changamoto zinazowakabili.

Waziri Mkuu amesema zao la parachichi ni miongoni mwa mazao yenye faida kubwa na linazalishwa kwa gharama nafuu, hivyo amewahimiza wananchi kulima zao hilo kwa ajili ya kujipatia fedha zitakazowawezesha kujikwamua kiuchumi.

Amesema zao la parachichi limechangia katika kutatua tatizo la ajira nchini, hivyo ametoa wito kwa Watanzania kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kuchakata zao hilo kwa kuwa linafaida kubwa.

Kadhalika, Waziri Mkuu amempongeza Bw. Mlimbira kwa kuwa na shamba kubwa la parachichi ambalo limewezesha kutoa ajira kwa wananchi wengi pamoja na kuwahamasisha walime zao kwa kuwagawia miche kwa gharama nafuu.





## WAZIRI MHAGAMA: JENGENI VIWANDA VYA VIRUTUBISHI VYA VYAKULA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Jenista Mhagama ameushauri ushirika wa wazalishaji wakubwa wa vyakula nchini kujenga viwanda vya kutengeneza Virutubishi vinavyoongezwa kwenye vyakula badala ya kuviagiza virutubishi hivyo nje ya nchi. Virutubishi hivyo ni madini ya chuma, Zinki, Asidi ya foliki na Vitamini B 12.

Waziri Mhagama ametoa wito huo baada ya kutembelea viwanda vya S.S Bakhresa Plant na Murzah Wilmar complex, 21st Century Food and Packaging, Lina Millers Ltd jijini Dar es salaam na Neelkanth Salt Ltd mkoani Pwani.

“Sisi kama serikali tupo tayari kushirikiana na nyie na tutatengeneza mazingira mazuri ya kuwawezesha kufanya uwekezaji wa viwanda hivyo. Tunaamini virutubishi hivi vikizalishwa hapa nchini gharama mnayotumia kununua virutubishi hivyo itapungua, lakini pia tutakuwa na uhakika

zaidi wa aina ya virutubishi tunavyotumia kwenye vyakula vyetu” Amesisitiza Mhagama.

Ameongeza kuwa uanzishwaji wa viwanda hivyo utaongeza ajira kwa watazania ambao bado wapo kwenye soko la ajira, pia amebainisha kuwa viwanda hivyo vitapunguza matumizi makubwa ya fedha za kigeni kwa kufanya manunuzi nje na fedha za kigeni zitaongezeka nchini kwa kuwa kuna nchi jirani ambazo wameamza kutekeleza sheria na Programu za kuongeza virutubishi hivyo zitakuja kununua virutubishi hivyo hapa nchini.

“Eneo, jingine ambalo tungependa mfikirie ni kutengeneza vifaa vya kurutubisha chakula (dosi-fier), mkiweza kuvitengeneza hivi vifaa hapa nchini na mkatumia nyie wenyewe lakini vikatumiwa na wasindikaji wa Kati na wadogo tutakuwa tumetengeneza vizuri mnyororo wa kuongeza virutubishi kwenye vyakula” Amesisitiza Mhagama.



## WATUMISHI OFISI YA WAZIRI MKUU WATAKIWA KUZINGATIA UZALENDO

Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu wameaswa kuzingatia uzalendo na matumizi sahihi ya rasilimali zinazotolewa ikiwemo fedha katika kutekeleza majukumu yao ili kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Tano .

Hayo yamesemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama Machi 12, 2021 Jijini Dodoma wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo.

“Tunapotekeleza majukumu yetu kwa uzalendo na weledi tunaonesha mfano bora kwa Wizara zote kama waratibu wa shughuli za Serikali na pia tunamsaidia Mhe. Waziri Mkuu katika utekelezaji wa shughuli zote za kila siku za Serikali hivyo niwaase kufanya kazi kwa bidii zaidi”, alisema Mhe. Mhagama

Amesema kuwa Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamataja Mhe. Waziri Mkuu kuwa Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali hivyo ni vyema kila mjumbe wa kikao cha baraza la wafanyakazi akazingatia kuwa Ofisi ina majukumu makubwa yakusimamia na kuratibu shughuli za kila siku.

Aidha, Mhe. Mhagama amewataka Wakuu wa Idara na Vitengo kuhakikisha wanatatua kero za wafanyakazi walio chini yao kwa wakati ili kuendelea kudumisha taswira nzuri ya Ofisi hiyo na pia kuwataka kuwa tayari kubadilika na kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia kwa kuweka mpango bora wa mafunzo unaogusa watumishi wote.

“Watumishi wote oneni kuwa mnachangamoto ya kuendelea kuzingatia uzalendo na weledi katika kupiga vita rushwa na ufidadi ili kuendelea kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kwa manufaa ya wananchi wote”



**KATIBU MKUU**  
**Ofisi ya Waziri Mkuu**  
**2 Mtaa wa Relini, S.L.P 980**  
**40480 Dodoma,**  
**Baruapepe: ps@pmo.go.tz, Simu:+255262322480**  
**Fax:+255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz**